HALIUZWI

# BUNDA Mji

HALMASHAURI YA MJI BUNDA

OKT - DEC, 2022

**Bunda Yetu, Maendeleo Yetu, Tuwajibike** | **TOLEO NO. 1**



# SHILINGI BILIONI 1.54 ZAJENGA MADARASA BUNDA MJINI

- **Madarasa 77 yamejengwa**
- **Shule 13 za Sekondari zimenufaika**
- **Zaidi ya wanafunzi 5041 kunufaika**

**Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# SHILINGI BILIONI 1.54 ZAJENGA MADARASA BUNDA MJI



Mnamo mwezi Septemba mwaka 2022, Halmashauri ya Mji wa Bunda ilipokea fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 1.54 toka Serikali kuu kwaajili ya ujenzi wa madarasa 77 ya sekondari.

Madarasa hayo ni kwaajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza watakaoingia mwaka 2023. Lengo la Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu wanapata nafasi ya kuendelea na elimu ya Sekondari.

Makadilio ya wanafunzi ambao walitarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 yalikua ni wanafunzi 6376 na kufanya upungufu wa vyumba vya madarasa ya sekondari kuwa 65 katika Halmashauri yote.

Halmashauri ya Mji wa Bunda inajumla ya shule za Sekondari 16 ambapo shule ya 16 ni shule mpya ilijongwa kwa fedha za SEQUIP shilingi milioni 470. shule hii ni shule ya kata ya Nyamakokoto na inatarajiwa kufunguliwa mwaka 2023.

Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan iliamua kulibeba suala la upungufu wa madarasa kwa shule za sekondari kwa kutenga shilingi Bilioni 800 za ujenzi wa madarasa nchi nzima.

Halmashauri ya Mji wa Bunda ni Miongozi mwa Halmashauri ambazo zimenufaika na fedha hizo kwa kupata shilingi Bilioni 1.54 za ujenzi wa madarasa 77.

Jumla ya shule 13 za Sekondari ambazo zilikua na uhitaji wa madarasa zimepata fedha kulingana na idadi ya uhitaji kama ifuatavyo;



Mchakato wa ujenzi wa madarasa haya haukua mwepesi kwani uliwafanya Viongozi wa Mkoa, Wilaya na Halmashauri kutokaa ofisini kufanya ufuatiliaji hadi ujenzi ulipokamilika.

Kwa upande wa Halmashauri ya Mji wa Bunda Uongozi wa Halmashauri ulishirikiana bega kwa bega na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuhakikisha ujenzi huu unakamiilika kwa wakati. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya Mhe. Joshua Nassari alikua akifanya ufuatiliaji kwa nafasi na ratiba yake wakati huo Mkurugenzi naye alikua akifanya ufuatiliaji wa kila siku kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa.

Ziara ya Viongozi wa Mkoa nazo zilikua hazikatikati kuangalia maendeleo ya ujenzi wa madarasa katika kila Halmashauri.

Wahenga walisema "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu". Msemo huu uliwafanya viongozi hawa kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha maagizo ya Serikali ya madrasa kukamilika kabla ya shule kufunguliwa yawe yamekamilika.

Mathalani, Wakuu wa shule kwa upande wao wamefanya kazi kubwa ya kusimamia ujenzi huo kiasi kwamba hata likizo waliisikilizia hewani hadi ujenzi utakapokamilika.

Kupitia Kmati mbalimbali za ujenzi zilizoundwa na Walimu wa shule husika zimesimamia kikamilifu ununuzi wa vifaa, mapokezi ya vifaa pamoja na matumizi yake na kuhakikisha hakuna hata kitu kimoja kinachohusu ujenzi kinapotea au kinacheleweshа ujenzi kukamilika.

Ujenzi huu umejengwa kwa njia ya FORCE ACCOUNT kwa kutumia mafundi uashi (Local fundi). jambo ambalo limepelekea kuzalisha ajira nyingi sana kwa mafundi wa ndani pamoja na vijana kupitia vibarua.

Hii imesaidia pia mzunguko wa fedha kuwa mkubwa katika Halmashauri ya Mji wa Bunda kwani fedha nyingi zimebaki ndani ya Halmashauri kuanzia kwa wauza bidhaa za ujenzi hadi mafundi.

Hadi kufikia sasa ujenzi umekamilika kwa shule zote 13 za sekondari. ikiwa ni sambamba na viti na meza 40 kwa kila darasasa kama maelekezo ya Serikalli yalivyokua yakielekeza.

Kwa mujibu wa Takwimu za Matokeo ya Darasa la saba 2022, jumla ya wanafunzi 5041 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023. wanafunzi wote hawa wamepangiwa shule na hakuna hata mmoja atakae kosa nafasi.

Uongozi wa Wilaya na Halmashauri ya Mji wa Bunda unatoa salamu za shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Halmashauri ya Mji wa Bunda fedha hizo za ujenzi wa madarasa na kuondoa changamoto ya wanafunzi wengi wanaofaulu na kukosa nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Kazi iendeleee...............................................





# NAIBU WAZIRI SILINDE AIPONGEZA HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA KWA KUZINGATIA UBORA WA MIRADI



Naibu Waizri Ofisi ya Rais Tamisemi Mheshimiwa David Silende (Mb) amefanya ziara ya kutembelea Miradi ya ujenzi wa maddarasa katika Halmashuri ya Mji wa Bunda ambapo ameipongeza Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa kutekeleza Miradi hii kwa ubora na kuzingatia thamani ya Miradi hiyo.

Mheshimiwa Silinde ametembelea shule mpya ya kata ya nyamakokoto inayojengwa kwa ufadhiri wa Mradi wa SEQUIP na pia ametembelea shule ya Sekondari Bunda.

Mheshimiwa Silinde amesema Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imedhamilia Suluhu kuondoa adha ya upungufu wa madarasa nchini na hivyo kuwafanya wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

Zaidi Naibu Waziri ameiagiza Halmashauri ya Mji wa Bunda kuhakikisha inakamilisha maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika Sekondari ya Nyamakokoto. Aidha amewahakikishia wananchi kwamba maboma hayo yatakamailika kwani fedha zipo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Joshua Nassari ameishukuru sana Serikali kwa kuleta fedha za ujenzi wa madarasa na shule mpya mbili Bunda Mjini na Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Nassari amesema ujenzi wa Shule mpya ya Nyamakokoto itaenda kusaidia kusaidia Kata zaidi ya moja hapa mjini zenye watoto wengi. Zaidi amesema Serikali ya awamu ya sita inaleta fedha nyingi sana za miradi jambo ambalo halijawahi kufanyika hapo nyuma.

Mheshimiwa Michael Kweka, Mwenyekiti wa Halmashuri ya Mji wa Bunda ametuma salamu za pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi mingi anayoileta Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Naye, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda Emmanuel Mkongo amesema siri ya kufanya vizuri katika miradi inayoletwa na Serikali Bunda Mji ni Umoja, Mshikamano na ushirikiano baina ya Watumishi na wawakilishi wa wananchi kwa maana ya Waheshimiwa Madiwani kupitia baraza la Halmashauri.

Mkurugenzi ameongeza kusema kuwa tayari Ofisi yake imetenga zaidi ya shilingi milioni 20 kwaajili ya kuendelea kukamilisha ujenzi wa shule hiyo mpya ya Nyamakokoto.

*Imendaliwa na LIWINA MNAMBA*

# MAKALA: Maisha ya Bi.Mariam na TASAF



"Kabla ya kujiunga na TASAF nilikua najishughulisha na kuuza viazi katika maeneo mbalimbali Musoma na hapa Bunda. Baadae nilipata tatizo la miguu nikawa siwezi kutembea umbali mrefu hivyo kushindwa kuendelea na shughuli yangu ya kuuza viazi, nikawa nipo nimekaa tu nyumbani. Maisha yalianza kuwa magumu kiasi kwamba nikawa nashindwa kumudu maisha yangu na wakati huo nilikua nalea wajukuu wangu wawili, watoto wa mdogo wangu ambao waliamua kunipatia baada ya kuona sina uwezo wa kupata mtoto." Anasema Bi. Mariam.

Bi Mariam Mwashi ni mzaliwa wa Kamgegi Wilaya ya Butiama na baadae mwaka 1991 aliamua kufanya maisha yake wilaya ya Bunda katika kata ya Nyamakokoto Halmashauri ya Mji wa Bunda. Elimu yake ni darasa la kwanza la zamani lakini anajua kusoma na kuandika. Anasema "Kiingereza ndio sijui lakini mengine yote, maandishi makubwa makubwa nakucharazia vizuri sana."

Baada ya kuhangaika kwa muda mrefu, Bi. Mariam anasema mwaka 2014 alibahatika kujinga na mfuko wa Tasaf ambao ndio ukawa kama mkombozi wa maisha yake. Bi. Mariam anasema fedha anazopokea kutoka Tasaf huwa anaweka kwenye mtaji wake.

Bi. Mariam kwa sasa anajishughulisha na utengenezaji wa majiko ya mkaa. Je, nani alimfundisha Bi. Mariam kutengeneza majiko hayo? "Ni Mungu, hakuna alienifundisha kutengeneza majiko. Huwa nalala naliaaa sina mtoto sina mume hata ndugu niliowalewa wamenitenga, nikiamka naanza kukorochoka kujifunza hadi nikajua. Jiko la kwanza kutengeneza ndio ninalolitumia hadi sasa." Anasema Bi. Mariam.

Majiko anayotengeneza anauza kuanzia shilingi 3,000/- hadi 60,000/- Wateja wa majiko haya kwa sasa wanaenda nyumbani kwake kwani hana sehemu ya kuuzia na anasema wateja wa majiko haya wapo wengi sana. "Makasha ya majiko haya huwa natengenezewa na mafundi wa vyuma chakavu waliopo barabara ya Ukerewe baada ya hapo huyatengeneza vizuri kwa kutumia udongo."

# MKURUGENZI MKONGO ATETA NA WALIMU WAKUU KUHUSU MATOKEO

Na Liwina Mnamba - Afisa Habari
Tarehe 08.12.2022

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Mji wa Bunda Ndg. Emmanuel Mkongo amesema hairdhishwi na matokeo mabaya ya wanayopata wanafunzi wa darsa la saba katika halmashauri ya Mji wa Bunda hivyo kuwataka Walimu Wakuu kuweka mikakati thabiti ya kuinua Elimu.

Ameyasema hayo katika kikao cha Umoja wa Walimu Wakuu Halmashauri ya Mji wa Bunda (TAPSHA) kilichofanyika katika ukumbi wa Kill Park Hotel.

Mkongo amesema ni wakati sasa Umoja wa Walimu Wakuu kukaa kwa pamoja kujadiliana mikakati itakayosaidia ufaulu mzuri kwa watoto wetu kwa maana mazingira ya mjini ni tofauti na kijijini hivyo matokeo yanatakiwa kuwa mazuri kwasababu mazingira yanaruhusu.

Kwa upande mwingine Mkurugenzi amewataka walimu kuendelea kubadilishana uzoefu wa kusimamia Miradi ya ujenzi hususani zile shule kongwe ambazo zinatarajiwa kupata fedha za BOOST za ukarabati. Aidha amewasisitiza kufanya kufanya mawasiliano na Ofisi yake pale wanapokua na wasiwasi wa kukamiiliaka kwa mradi kutokana na fedha na maelekezo waliyopewa kuliko kuanza na kuishia katikati.

Kuhusu changamoto ya Madawati, Mkurgenzi amesema Ofisi yake inatambua changamoto hiyo na tayari imeanza kulifanyia kazi na sasa ipo kwenye mawasiliano na mbunge Mhe. Robert Chacha Maboto kupitia fedha za mfuko wa jimbo kuona ni namna gani inaweza kupunguza changamoto hii kwa kutengeneza madawati na kuyagawa mashuleni.



Mwisho Mkurugenzi amewataka Walimu wakuu kupitia Umoja wao kuwasilisha Ofisini kwake mapendkezo yao yatakayorahisisha utendaji kazi wao wa kila siku katika kutekeleza majukumu yao. lakini pia kuwasilisha hali ya ikama ya walimu katika ofisi zao ilikuona maendeo yenye upungufu mkubwa wa walimu ili yafanyiwe kazi.



# DR. MASHINJI AWAKUMBUSHA WAZAZI UMUHIMU WA LISHE KWA WATOTO

KAIMU Mkuu wa Wilaya ya Bunda ambae pia ni Mkuu wa wilaya ya Serengeti Dr. Vincent Mashinji amewakumbusha wazazi na viongozi wa Wailaya ya Bunda umuhimu wa Lishe bora kwa watoto hasa katika makuzi yao. ameyasema hayo katika kikao cha Wakuu wa Idara ya Halmashauri ya Mji wa Bunda na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda wakati wa maandalizi ya bajeti za lishe 2023/24.

“Ubongo wa ulio nao sasa asilimia 95 uliupata ukiwa na umri chini ya miaka mitano” maneno ya Dr. Mashinji wakati akidavua umuhimu wa lishe katika kikao hicho. Dr. Mashinji amesema tatizo la lishe kwasasa linaonekana kuwa kubwa na ndio maana unakutana wazazi wanahangaika sana kuwaelekeza na kuwafundisha watoto wao mambo mbalimbali.

Aidha Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ameweka bayana kuwa takwimu zinaonesha zaidi ya watoto laki moja na nusu Wilayani Bunda wamedumaa, hivyo tatizo hili ni kubwa na jitihada za lazima zinahitajika kukabiliana nalo.

Manthalani, Dr. Mashinji amesisitiza sana matumizi ya vyakula vyenye madini ya FOLIC ACID na IODINE kwa watoto ili kuwafanya kuwa na afya njema ya akili na iliyobora.

Baada ya kufungau kikao hicho wataalamu toka Wizarani na Mkoani pamoja na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda na Halmashauri ya Wilaya waliendelea na Kikao cha majadiliano ya namna gani ya kupanga bajeti ya lishe iliyobora na inayolenga kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la lishe duni katika Wilaya ya Bunda na Mkoa wa Mara kwa ujumla.

Kabla ya kupanga Bajeti ya Lishe kwa mwaka 2023/24. Wajumbe walifanya tathimini ya bajeti iliyopita ya lishe kuona mapungufu na kuyaepuka katika najeti ijayo.

Na Liwina Mnamba - Afisa habari
tarehe 14.11.2022





# DC NASSARI ATATUA MGOGORO ZANZIBAR

Na Liwina Mnamba
Tarehe 19.12.2022

MKUU wa Wilaya ya Bunda Mhe. Joshua Nassari ametatua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu baina ya Mwenyekiti wa mtaa wa Zanzibar kata ya Nyasura dhidi ya wananchi wake. Baadhi ya wananchi wa mtaa wa Zanzibar wamekua wakimlalamikia Mwenyekiti wao kuwa na ushirikiano duni katika mtaa wake hali iliyopelekea wananchi kugoma kushiriki katika shuguli za maendeleo na ulinzi shirikishi katika mtaa wao.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili za mlalamikiwa na walalamikaji, Mhe. Nassari ametoa maelekezo kwamba Mwenyekiti ataendelea kuwa mwenyekiti wa mtaa huo wakati taratibu nyingine za kiuchunguzi zikiendelea na endapo itabainika kwamba mwenyekiti anahusika na madai ya walalamikaji basi hatua za kisheria zitachukuliwa.





Aidha, Mheshimiwa Nassari amewataka wananchi pamoja na mwenyekiti wao kuondoa tofauti zao na kujumuika kwa pamoja kufanya shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kumalizia ujenzi wa maboma mawilia ya madarasa ya shule ya msingi Kilimani uliokwama kutokana na tofauti hizo.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya amemuelekeza Mkurugenzi wa Halmasauri ya Mji wa Bunda kufanya mabadiliko ya vituo vya kazi kwa kumhamisha mtendaji wa mtaa wa Zanzibar kwenda mtaa wa Nyasura A na wa Nyasura A kwenda mtaa wa Zanzibar ili kuweka taratibu za kiutawala vizuri katika eneo hilo.

Wananchi walikuwa wakimlalamikia mwenyekiti kuwa na makundi yaliyopelekea asitende haki kwa baadhi ya wananchi wengine, pili amekua akipuuza suala la usalama ikiwemo kutotoa ushirikiano pindi yowe inapopigwa na zaidi wananchi kutofahamu hatima ya kesi za wizi zinakamatwa mtaani na kupelekwa kwake. Mwenyekiti alikiri kuyapokea malalamiko hayo na kusema sivyo yanavyotafsiriwa na wananchi wake.

# BAADHI YA MADARASA YALIYOJENGWA KWAAJILI YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023


Bunda sekondari madarasa 2


Nyiendo sekondari madarasa 4


Manyamanyama sek madarasa 5


Sazira Sekondari madarasa 8


Rubana sekondari madarasa 10


Dr. Nchimbi sekondari madarasa 10

HALIUZWI


NDG. EMMANUEL J. MKONGO
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA
td@bundatc.go.tz

LIWINA MNAMBA
MKUU WA KITENGO
MAWASILIANO SERIKALINI
+255 765 889 459